Maine Center for Disease Control and Prevention
An Office of the Department of Health and Human Services

**Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara--ukurasa wa 19**

**Ikiwa ninastahiki kusajiliwa kwa mpango wa WIC, ninaweza kupata manufaa kwa muda gani?**

- Wakati wa ujauzito
- Hadi mwaka mmoja baada ya kujifungua ikiwa unamnyonyesha mtoto wako
- Hadi miezi sita baada ya kujifungua ikiwa hunyonyeshi
- Hadi mwaka wa tano baada ya kumzaa mtoto

**Je, nikihama?**

Ikiwa unapanga kuhamia sehemu nyingine huku Maine, unaweza kuangalia kwenye tovuti yetu ili kupata orodha ya ofisi zote za WIC kwenye jimbo katika **www.wicforme.com**. Ikiwa unapanga kuhama Maine, tafadhali julisha wafanyakazi wa WIC.

**Wakala ni nani?**

Wakala ni mtu unayemwamini. Unampa mtu huyu ruhusa ya kutumia hundi zako za WIC kwenye duka la mboga na matunda au kuhudhuria ziara za WIC kwa niaba yako. Ikiwa utateua mtu fulani awe wakala, mtu huyo ni lazima:

- Atie sahihi kwenye sehemu ya nyuma ya folda hii ya WIC
- Ailete dukani anapotumia hundi za WIC
- Afahamu ni vyakula gani atanunua na jinsi ya kutumia hundi za WIC
- Alete folda hii wakati wa ziara ya WIC pamoja na fomu ya utambulisho

**Ni kwa nini wafanyakazi wa WIC hawawezi kuzungumza na wanafamilia wengine au marafiki zangu kuhusu mtoto wangu au kunihusu?**

Mpango wa WIC hulinda haki yako ya ufaragha. WIC haitashiriki taarifa zozote bila idhini yako. Hii ni pamoja na nyakati za miadi na taarifa za kimatibabu. Hata hivyo, ikiwa mfanyakazi wa WIC anaamini kuwa mtoto yuko hatarini, anahitajika kisheria kuripoti hili kwa mfanyakazi wa DHHS ambaye atafuatilia suala hilo na familia.

**Na je, hundi zangu za WIC zikipotea, zikiibiwa au zikiharibika?**

Julisha ofisi ya WIC mara moja. Zishughulikie hundi zako za WIC kama pesa taslimu. Ziweke kwenye mahali salama.

Maine Center for Disease Control and Prevention
An Office of the Department of Health and Human Services

**Je, ninahitaji kununua kila kitu kilichoorodheshwa kwenye hundi yangu ya WIC?**

Hapana, hauhitajiki kununua kila kitu kilichoko kwenye hundi yako ya WIC. Nunua vyakula ambavyo unajua utahitaji.

**Je, nikitumia hundi zangu zote za WIC na chakula cha mtoto wangu mchanga kiishe?**

WIC inaweza kutoa tu kiasi fulani cha chakula cha mtoto kila mwezi. Umri wa mtoto wako unapoongezeka, anaweza kuhitaji chakula kingi zaidi ya kile unachopokea kutoka kwa WIC. Hili likitokea, utahitajika kununua chakula cha ziada cha mtoto hadi utakapopokea hundi za WIC zinazofuata.

**Je, ninaweza kushiriki kwa zaidi ya mpango mmoja wa WIC kwa wakati mmoja?**

Hapana.

**Ni kwa nini wafanyakazi wa WIC hawawezi kuzungumza na wanafamilia wengine au marafiki zangu kuhusu mtoto wangu au kunihusu?**

Mpango wa WIC hulinda haki yako ya ufaragha. WIC haitashiriki taarifa zozote bila idhini yako. Hii ni pamoja na nyakati za miadi na taarifa za kimatibabu. Hata hivyo, ikiwa mfanyakazi wa WIC anaamini kuwa mtoto yuko hatarini, anahitajika kisheria kuripoti hili kwa mfanyakazi wa DHHS ambaye atafuatilia suala hilo na familia.

**Na je, hundi zangu za WIC zikipotea, ziibiwe au ziharibike?**

Ijulishe ofisi ya WIC mara moja. Zishughulikie hundi zako za WIC kama pesa taslimu. Ziweke kwenye mahali salama. **What if i lose my** .

**Je, ninahitaji kununua kila kitu kilichoorodheshwa kwenye hundi yangu ya WIC?**

Hapana, hauhitajiki kununua kila kitu kilichoko kwenye hundi yako ya WIC. Nunua vyakula ambavyo unajua utahitaji.

**Je, nikitumia hundi zangu zote za WIC na chakula cha mtoto wangu mchanga kiishe?**

WIC inaweza kutoa tu kiasi fulani cha chakula cha mtoto mchanga kila mwezi. Umri wa mtoto wako unapoongezeka, anaweza kuhitaji chakula kingi zaidi ya kile unachopokea kutoka kwa WIC. Hili likitokea, utahitajika kununua chakula cha ziada cha mtoto hadi utakapopokea hundi za WIC zinazofuata.